
# KIJITABU CHA WAISLAM KUHUSU COVID-19

MWONGOZO WA JINSI YA KUKABILIANA NA GONJWA LA COVID-19 KWA MTAZAMO WA KIISLAMU

KIMECHAPISHWA KWA MASHAURIANO YA WANAZUONI WA NGAZI ZA JUU NA MADAKTARI WA TIBA







SPIRITUAL ANTIDOTE

# Yaliyomo


### *Utangulizi*

3 Utangulizi

4 Nyakati Dhahabia

### *Hatua za Kujikinga*

5-7 Ulinzi wa kiroho

8 Hatua za kiutendaji

### *Kuonekana Dalili*

9 Hatua za kuchukua zikionekana dalili

10 Kuwa na fikra chanya na jikurubishe kwa Mwenyezi Mungu

11 Du’a za Mtume za kusoma wakati unaumwa

12 Kusaidia watu wenye dalili

### *Dalili zikizidi kuwa mbaya*

12 Kabla ya kwenda hospitalini

12 Hatua tatu muhimu za kuchukua

13-14 Kufanya toba Kamili

15-16 Kuswali kama mgonjwa

17-19 Vidokezo vya kukuwezesha kumfikiria vyema Mwenyezi Mungu

### *Hospitalini*

20 Mambo ya kufanya ukiwa hospitalini

20 Ikiwa utapona kutoka kwa ugonjwa

20 Wakati wa hali taabani

20 Kuwa peke yako

21 Umuhimu wa La illah illa-Allah

### *Kushughulika na kifo*

22-24 Hatua za kwanza kuchukua wakati unapata taarifa

25 Kuwasaidia watu walipatwa na msiba

### *Taratibu za Mazishi*

26 Kuosha mwili wa marehemu

26 Kukafini mwili wa marehemu

27-28 Swala ya jeneza

29 Kuzika

29 Baada ya mazishi

### *Baada ya Mazishi*

30 Kuzuru kaburi

30 **Neno la mwisho**

# UTANGULIZI

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

*Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwingi Wa Rehema Mwenye Kurehemu.*

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu. Tunaomba msaada kwake, baraka na uongofu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amrehemu Mtume Muhammad, amlinde na amuinue katika daraja la juu.

Mlipuko wa janga la corona umeenea haraka ulimwenguni kote, na kubadili kabisa hali za maisha ya watu. Hii pia inajumuisha jamii ya kiislamu, ambayo imeathirika kwa njia tofauti.

Kwa kuandika kijitabu hiki, tunadhamiria kuleta matumaini kwa jamii kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kutoa vidokezo vya vitendo ambavyo vimewekwa katika kanuni na maarifa sahihi ya Uislam.

Malengo ya kijitabu hiki ni:

- Kuimarisha imani zetu na mauhusiano yetu ya kiroho na Mwenyezi Mungu katika wakati huu.
- Kuhakikisha tuko tayari kukabiliana na matukio yote juu yetu na wapendwa wetu.

Mwenyezi Mungu aufanye wakati huu wakati ambao tunakuwa karibu zaidi naye. Tunaomba atulinde, wapendwa wetu na jamii kwa ujumla kutokana na madhara. Mwishowe, tunamwomba awasamehe wale wote ambao wametangulia na awe na huruma juu yao.

# Nyakati Dhahabia



**Mtume ﷺ alituambia:**

" *Yule anayekaa katika ardhi yao wakati wa tauni* akawa na subira,* akatafuta thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, akijua kabisa kuwa hakuna kitakachomsibu isipokuwa kile ambacho Mwenyezi Mungu alimkadiria; atapewa thawabu kama ile ya shahidi "


[Saheeh Al-Bukhari (3474)]

**Wanazuoni wengi wamesema kwamba janga hili linakuja chini ya* hukumu ya ugonjwa wa tauni. Tunatumai kuwa Mwenyezi Mungu, kwa ukarimu wake, atawalipa wale wanaofuata masharti haya kama Yeye angewalipa waathirika wa janga la tauni

## Ili kupata fadhila hii kubwa mtu anahitaji:




**1. Abaki sehemu husika**



**2. Awe na subira**



**3. Atafute fadhila za Mwenyezi Mungu**



**4. Aamini kwamba hakuna kitu kitakachompata isipokuwa kile ambacho Mwenyezi Mungu amekadiri**

## Hadithi hii inahusu makundi matatu ya watu:



Mtu anayekufa kutokana na ugonjwa huo



Mtu ambaye hupona kutokana na ugonjwa huo



Mtu ambaye hakuupata ugonjwa huo wakati wote

[Fathul Bari (1/538)]

# HATUA ZA KUJIKINGA

## Ulinzi wa kiroho

**Kuswali Fajr kwa wakati**

Mtume ﷺ amesema:
"Yeyote anayeswali Fajr yuko kwenye ulinzi wa Mwenyezi Mungu."

[Saheeh Muslim (657)]



**Kuswali Dhuha**

*Mwenyezi Mungu amesema: "Ewe Mwana* wa Adamu nifanyie rakaa nne (swala ya Dhuha) mwanzoni mwa siku; Nitakutosheleza kwa sehemu nyingine ya siku yako."

[At-Tirmidhi (475) na imethibitishwa na Adh-Dhahabi kwenye As-Siyar (8/323)]

*NB: Wakati wa Dhuha huanza baada ya* kuchomoza kwa jua na kumalizika dakika 10 kabla ya wakati wa Dhuhr kuanza, inaswaliwa katika rakaha mbili)

### Du'a ya Mtume ya kusoma kabla ya kutoka nyumbani

بِسْمِ اللَّهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ،وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

Bismillaahi tawak'kaltu 'alAllaah, wa laa hawla wa laa quwwata illaa billaah
Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, ninaweka tumaini langu na kumtegemea Mwenyezi Mungu, na hakuna nguvu ya kufanya mema wala nguvu yoyote ya kujizuia na mabaya isipokuwa Kwa (Msaada wa) Mwenyezi Mungu

"Yeyote anayesoma hii (dua), ataambiwa, 'Umeongoka, umetoshelezwa (yaani mahitaji yako yameshughulikiwa), umelindwa' na Shaytan atakwenda mbali sana na mwenyewe."

[Abu Dawood, (5095) & imethibitishwa na Ibn Al-Qay'yim kwenye Zad Al-Ma'ad (2/335)]

### Du'a ya mtume ya kuhifadhi baraka

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ زَوَالِ نِعْمَتِكَ ، وَتَحَوُّلِ عَافِيَتِكَ ، وَفُجَاءَةِ نِقْمَتِكَ
وَجَمِيعِ سَخَطِكَ

Allaahumma innee aʿoodhu bika min zawaali niʿmatik, wa tahaw-wuli ʿaafiyatik, wa fujaa'ati niqmatik, wa jameeʿi sakhatik

Mwenyezi Mungu najikinga kwako na kuondokewa na rehema zako, ulinzi wako na uzima ulionipa kugeuka kuwa shida na maradhi, na adhabu zako za ghafla na chochote ambacho kitakuletea kughadhabika

[Saheeh Muslim (2739)]

# HATUA ZA KUJIKINGA

## Ulinzi wa kiroho

### Du'a ya Mtume kwa ajili ya ulinzi dhidi ya magonjwa

اللّٰهُمَّ إِنِّي أَعُوْذُ بِكَ مِنَ الْبَرَصِ وَالْجُنُونِ وَالْجُذَامِ وَمِنْ سَيِّئِ الْأَسْقَامِ

Allaahumma innee a'oodhu bika minal bara<u>s</u>i wal-junooni wal-judhaami wa min say'yi' il-asqaam

Mwenyezi Mungu, najikinga kwako na lukemia, na kuchanganyikiwa, na ukoma, na maradhi  yote mabaya.

[Abu Dawood (1554) & imethibitishwa na An-Nawawi kwenye Al-Adhkar (p.483)]

### Du'a ya Mtume kwa ajili ya ulinzi dhidi ya majanga

اللّٰهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ جَهْدِ الْبَلَاءِ، وَدَرَكِ الشَّقَاءِ، وَسُوْءِ الْقَضَاءِ، وشَمَاتَةِ الْأَعْدَاءِ

Allaahumma innee a'oodhu bika min jahdil balaa', wa darakish'shaqaa', wa soo-il qa<u>d</u>aa', wa shamaatatil 'a-daa'

Ewe Mwenyezi Mungu, natafuta ulinzi wako kutokana na shida za misiba, kutoka kwa hatma mbaya, kutoka mwisho mbaya na kutoka kwa furaha mbaya ya  maadui.

[Saheeh Al-Bukhari (6347)]

### Du'a ya Nabii Yunus

لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ

Laa ilaaha illaa anta sub<u>h</u>aanaka innee kuntu min a<u>dh</u>'<u>dh</u>aalimeen

Hakuna anayestahili kuabudiwa ila Wewe, Wewe ni kamili na juu ya upungufu wowote, hakika  mimi nilikuwa katika wenye kutenda makosa madhalim

Mtume ﷺ amesema: " Hakuna Mwislamu asemayo du'a hii juu ya chochote, lakini Mwenyezi Mungu atajibu maombi yake."

[Surah Al-Anbiya:87] & [At-Tirmidhi (3505) & imethibitishwa na Ibn Hajr; Al-Futuhaat Ar-Rabaaniyyah (4/11)]

# HATUA ZA KUJIKINGA

## Ulinzi wa kiroho

### Dua ya Mtume ya kusoma asubuhi na jioni

*Wakati wa dhikri ya* asubuhi ni kati ya Fajr na jua kuchomoza, na wakati wa ajili ya zikr za jioni ni kati ya ' Asr na Maghrib

بِسْمِ اللّٰهِ الَّذِي لَا يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيْمُ

Bismillaahil ladhi la yadur'ru ma'asmihi shay'un fil-ardi wa la fis'samaa'i wa huwas-samee'ul 'aleem

Na kwa jina la Mwenyezi Mungu ambao kwa jina lake likitajwa, hakuna kitu kinacho weza kudhuru kwenye ardhi wala katika mbingu, naye ni mwenye kusikia, mwenye kujua.

"Yule anatakayesoma dua hii mara tatu asubuhi na jioni, hakuna chochote kitakachomdhuru."

[At-Tirmidhi (3388) & authenticated by him]

اللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، اَللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَفْوَ وَالْعَافِيَةَ فِي دِينِي وَدُنْيَايَ وَأَهْلِي، وَمَالِي، اَللّٰهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِي،وَآمِنْ رَوْعَاتِي،اَللّٰهُمَّ احْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَيَّ، وَمِنْ خَلْفِي، وَعَنْ يَمِينِي،وَعَنْ شِمَالِي،وَمِنْ فَوْقِي، وَأَعُوذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي

Allaahumma innee as-alukal 'aafiyata fid'dunyaa wal aakhirah, Allaahumma innee as-alukal 'afwa wal'aafiyata fee deenee wa dunyaaya wa ahlee wa maalee, Allaahum'mastur 'awraatee wa aamin raw'aatee, Allaahummahfadhnee min bayni yaday'ya, wa min khalfee wa 'an yameenee wa 'an shimaalee, wa min fawqee, wa a'oodhu bi'adhamatika an ughtaala min tahtee


Ewe Mwenyezi Mungu, nakuomba unipe usalama  ustawi na ulinzi katika ulimwengu huu na Akhera. Ewe Mwenyezi Mungu, nakuomba msamaha kwa mapungufu yangu, na unijalie usalama, amani na ulinzi wa imani yangu, mambo yangu ya kidunia, familia yangu na utajiri wangu. Ewe Mwenyezi Mungu, ficha makosa yangu na unilinde kutokana na yale ambayo yananipa wasiwasi. Ewe Mwenyezi Mungu, nilinde kutoka kwa yaliyo mbele yangu na yaliyo nyuma yangu, kutoka kulia kwangu na kushoto, na kutoka juu yangu, na ninakimbilia kwako ili nisije nikaangamizwa kutoka chini yangu

Kusomwa asubuhi mara moja na jioni mara moja.


[Abu Dawood (5074) & imethibitishwa na An-Nawawi kwenye Al-Adhkar (p.111)]]

# HATUA ZA KUJIKINGA


## Hatua za kiutendaji

| | |
|---|---|
|  | **1. Epuka sehemu yeyote ile ambayo mtu anaweza kuambukiza ugonjwa** |
|  **Baki Nyumbani** | **2. Usitoke nje mpaka kuwe na umuhimu sana**<br>• Kama utahitajika kwenda nje, toka mara chache |
|  | **3. Tekeleza umbali kati yako na watu wengine**<br>“Toroka ukoma vile utakavyomtoroka simba.”<br>[Saheeh Al-Bukhari (5707)]<br>• Ikiwa unataka kitu chochote kwa mtu, basi acha huo mzigo mlangoni kwao bila kugusa chochote<br>• Kaa umbali wa mita 2 kutoka kwa wengine unapokuwa nje |


### Kama ikihitajika ukatoka nyumbani...



**A. Vaa vifaa vya kinga na baadaye uvitupe sehemu usalama**




**B. Epuka kugusa mdomo wako, macho au pua**



**C. Takasa mikono yako safisha mara tu utakapofika nyumbani**

# KUONEKANA DALILI





## Hatua za kuchukua zikionekana dalili



### KUJITENGA!

**Ikiwa wewe au wapendwa wako mnaonyesha dalili zozote za ugonjwa huo, ni muhimu kujitenga mapema iwezekanavyo ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa**

## Vitu vya kufanya wakati umejitenga...

| | | |
|---|---|---|
|  **Swali sunna za ziada** |  **Soma Quran** |  **Sikiliza mawaidha** |
|  **Tafakari** |  **Mkumbuke Mwenyezi Mungu & fanya du’a** |  **Soma vitabu vyenye faida** |
|  **Wasiliana na familia** |  **Mazoezi** |  **Jifunze vitu vipya kwenye mtandao** |
|  **Pumzika na kunywa maji mengi** | Weka tumaini lako kwa Mwenyezi Mungu, chukua hatua juu ya mwongozo wa wataalamu wa huduma za afya na usiruhusu hofu ikucheleweshe kutafuta msaada wa haraka, ikiwa unahitajika. | |

# KUONEKANA DALILI

## Kuwa na fikra chanya na jikurubishe kwa Mwenyezi Mungu

### Inaweza kufuta dhambi zako!

*Mtume ﷺ alisema: "...janga* litaendelea kumpata mtu hadi atembee ardhini bila dhambi"

[At-Tirmidhi (2398) & imethibitishwa na mwenyewe]

### Ishara ya upendo wa Mwenyezi Mungu

*Mtume ﷺ alisema:* "Mwenyezi Mungu akimpenda mtu, humjaribu"

[At-Tirmidhi (2396) & imethibitishwa na Ibn Muflih in Al-Adaab Ash-Shar'iyyah (2/181)]

### Labda Mwenyezi Mungu anayo safu maalum inayokusubiri katika pepo

*Mtume ﷺ alisema:"... Hakika mtu ana* hadhi (maalum) na Mwenyezi Mungu ambayo haiwezi kupata kupitia vitendo vizuri, basi Mwenyezi Mungu anaendelea kumjaribu na kile ambacho mtu huyo hakukipenda hadi atakapata

[Saheeh Ibn Hibaan (2908) & imethibitishwa na Al-Haitami in Az-Zawajir (1/164)]

### Katika maisha yanayofuata, wengi watatamani wangejaribiwa katika ulimwengu huu

*Mtume ﷺ alisema: "Katika maisha yafuatayo, wale ambao walikuwa* salama, walikuwa na ustawi na ulinzi watatamani ngozi zao zingekuwa zimekatwa na mkasi, wakati huo watakapoona ujira mkubwa wa wale ambao walikuwa na majanga."

[At-Tirmidhi & imethibitishwa na As-Suyuti in Al-Jami As-Sagheer (7721)]

# KUONEKANA DALILI

## Du’a na ruqya za Mtume za kusoma wakati unaumwa

### Soma Surah Al-Fatihah

Surah Al-Fatihah ni mfumo wa tiba.

[Saheeh Al-Bukhari (2276)]

### Du’a  kwa ajili ya kuponya ugonjwa

اللّٰهُمَّ رَبَّ النَّاسِ أَذْهِبِ الْبَاسَ، وَاشْفِ أَنْتَ الشَّافِي، لَا شِفاءَ إِلَّا شِفَاؤُكَ، شِفَاءً لَا يُغَادِرُ سَقَمًا

Allaahumma Rabban-naasi adh-hibil bas, washfi antash-shaafi, laa shifaa-a illaa shifaa-uk, shifaa-an laa yughaadiru saqamaa

Ee Mola wa wanadamu! Ondoa uchungu, ondoa usumbufu, Ponya maumivu haya kwani Wewe ndiye unayeponyesha. Hakuna tiba isipokuwa ile ambayo imetolewa na Wewe, toa tiba ambayo haitoacha nyuma uchungu wowote au usumbufu wowote

[Saheeh Al-Bukhari, (5351)

### Du'a kwa ajili ya kuondoa maumivu

بِسْمِ اللّٰهِ

Bismillaah

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kuomba msaada wake, baraka zake na ulinzi wake

NB: Weka mkono wako ambapo unahisi maumivu na soma mara 3 kwa Kiarabu.

أَعُوذُ بِاللّٰهِ وَقُدْرَتِهِ مِنْ شَرِّ مَا أَجِدُ وَأُحَاذِرُ

A’oodhu billaahi wa qudratihi min sharri maa ajidu wa uhaadhir

Naomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu na nguvu yake kutokana na machungu ambayo ninapata na ambayo ninaogopa.

NB: Weka mkono wako ambapo unahisi maumivu na soma mara 7 wa kiarabu.

[Saheeh Muslim, (2202)]

# KUONEKANA DALILI

## Kuwasaidia watu wenye dalili

1. Tumuombe Mwenyezi Mungu awaponye

2. Tuwaombe wengine wafanye du'a kwa ajili yao *

* An-Nawawi alinukuu makubaliano juu ya kukubalika kwake
[An-Nawawi kwenye Al-Adhkar (p.643)]

3. Toa sadaka kwa ajili yao kwa tumaini kwamba Mwenyezi Mungu atawaponya (chakula, nguo, nk.)
[Saheeh Muslim (901)]

4. Wasaidie kwa njia yoyote ile, wakati ukihakikisha usalama wako na wengine

5. Kuwaweka katika hali nzuri, kamili na ya matumaini

# DALILI ZIKIZIDI KUWA MBAYA

## Kabla ya kwenda hospitali

### Hatua tatu kuu za kuchukua:

Daima ni bora kuwa tayari kuliko kutojitararisha. Kuchukua tahadhari sahihi katika hatua hii itahakikisha kwamba mtu anaawacha watu wa nyumbani bila masikitiko.

**1. Achia familia yako ushauri wowote ambao utakuwa na faida kwao**



**2. Fanya toba kamili (angalia kurasa zifuatazo kwa malezo zaidi)**



**3. Andika wosia kwa familia yako na waambie kile unachopenda kifanyike baada yako**



# WAKATI DALILI ZINAKUWA MBAYA ZAIDI

## Kufanya toba kamili

**Toba ya ujumla**

Kufanya toba ya jumla huhakikisha msamaha kwa dhambi zote za mtu, hata kama hawakumbuki kila dhambi, ikiwa:

1- kama wangekumbuka hiyo dhambi, wangetubu

2- mtu huyo hana upendo au unganisho katika dhambi hiyo

- **Ibn Taymiyyah**

[Al Fataawa Al-Kubra (5/279)]

## Toba ina sehemu kuu mbili:

### 1) Haki ya Mwenyezi Mungu


Masharti ya Haki za Mwenyezi Mungu:



1. Uwe mwaminifu kwa Mwenyezi Mungu





2. Acha kuifanya hiyo dhambi



3. Jutia kuifanya hiyo dhambi



4. Kuwa na maazimio makali kutoirudia hiyo dhambi



5. Kabla ya kufikiwa na malaika wa mauti

[Sharh Muslim na An-Nawawi (9/20-21), Al-Madaarij (1/192) & Tafseer Ibn Kathir (2/236)]

# WAKATI DALILI ZINAKUWA MBAYA ZAIDI

## Fanya toba kamili

### 2) Haki za viumbe

Inahitaji masharti yaliyoainishwa kwenye ukurasa uliopita pamoja na makubaliano na mtu yeyote ambaye umemkosea katika aina mbili zifuatazo :

### A. Umiliki

- Ikiwa umechukua au kukopa kitu ambacho ni cha mtu mwingine basi lazima ukirejeshe.
- Ikiwa hauna tena, basi rudisha thamani sawa na ulichochukua.
- Ikiwa kutoa thamani sawa haiwezekani, basi rudisha thamani ya sasa katika pesa.
- Ikiwa mwenyewe amefariki , basi apewe mrithi wake.
- Ikiwa hakuna njia ya kuwasiliana na mrithi au mmiliki huyo, toa pesa hizo sadaka kwa niaba ya mmiliki (ikiwa ni Waislamu).
- Kama si Waislamu, basi toa kama sadaka (lakini haipaswi kuwa kwa niaba yao).

### B. Heshima

- Unahitaji kuomba msamaha kutoka kwa mtu yeyote ambaye umemkosea, kivitendo au kwa maneno, n.k. kuapa, kusengenya, kutusi
- Ni bora kumuomba muhusika mweyewe msamaha moja kwa moja.
- Hata hivyo, unaweza kumfanyia du'a mtu na kumwomba Mwenyezi Mungu amsamehe ikiwa:
  1) mtu huyo hajui kuwa umemkosea / kuomba msamaha kutasababisha athari mbaya kuliko nzuri
  2) hakuna njia ya kuwasiliana nae
- Andika rasimu ya ujumbe au maelezo ya sauti ili kutuma kwa watu haraka iwezekanavyo. Unaweza kuwasaidia jamaa wazee ambao wanahitaji kufanya hivyo kwa kuandika ujumbe kwa ajili yao.
- Mfano wa ujumbe: “Naamini labda nilikuwa nakusengenya na kukuongelea vibaya juu yako, hivyo tafadhali naomba unisamehe…”

# WAKATI DALILI ZINAKUWA MBAYA ZAIDI

## Kuswali kama mgonjwa

Mtume ﷺ amesema: “Kitendo cha kwanza ambacho mtu atashughulikiwa Siku ya Kiyama itakuwa swala yake. Ikiwa ni nzuri basi atakuwa amefanikiwa , lakini ikiwa ni mbaya basi atakuwa mwenye kuangamia."

[At Tirmidhi (413) & imethibitishwa na An-Nawawi kwenye Al-Majmoo' (4/55)]

Kwa hiyo ni muhimu sana mtu kutozembea kutelekeza swala wakati huu mgumu

**Tafadhali hakikisha unafungasha yafuatayo katika mfuko wako wa kuendea nao hospitali**

- Simu Janja (yenye dira na app za swala)
  - Mfano; kupiga simu ya video, kuweka chaji, kutumia app ya swala, nk.
- Jiwe la kutayammum
  - Jiwe lolote linaweza faa
- Msala, sabuni, dawa ya mswaki, nguo za akiba, ndala na nk



### Udhu & Kutayammum

Fanya wudu ikiwa unapata maji au kwa maji yoyote yatakayoletwa kwako.

Ikiwa umevaa kofia ya oksijeni na haiwezi kuondolewa, inatosha kuipapasa wakati wa udhu.

**Fanya tayammum kama una kimoja au zaidi ya hivi vifuatavyo:**

- Huna njia ya kupata maji
- Huna chanzo cha maji.
- Kutumia maji kutafanya ugonjwa kuwa mbaya zaidi au kuchelewesha ahueni yako

**Kutayammum...**

**1**



**Papasa mikono yako juu ya jiwe la tayammum**

**2**




**Halafu papasa uso wako**

**3**



**Papasa mikono yako juu ya jiwe la tayammum tena**

**4**



**Halafu papasa mikono yako yote mpaka kwenye kiwiko. Tayammum itakuwa tayari**

[As-Sunan Al-Kubra by Al-Baihaqi (1/206)]

# WAKATI DALILI ZINAKUWA MBAYA ZAIDI

## Kuswali kama mgonjwa

### Namna ya kuswali...

Swali kwa kusimama kama kawaida.

Kama huwezi, Swali huku umekaa.

Ikiwa huwezi kukaa, basi swali umelala ukitazama qiblah - upande wowote ulio rahisi. Ikiwa pande zote mbili ni sawa, basi upande wa kulia ni bora zaidi.

Ikiwa hiyo haiwezekani, basi swali umelalia mgongo wako, na miguu yako kuelekea qiblah (ikiwezekana), vinginevyo unaweza kuswali ukiwa umelala upande wowote.

### Jinsi ya kufanya rukuu na sujudu kama unaswali ukiwa umekaa...

- Inamisha kichwa chako mbele na mgongo wako chini kwa rukoo na sujudu kama una uwezo
- Ikiwa huwezi kupinda mgongo wako, basi inamisha kichwa chako kitatosha

### Jinsi ya kufanya rukuu na sujudu kama unaswali ukiwa umelala...

- Inamisha kichwa chako kwa rukuu na sujudu
- Tofautisha kati ya sujudu na rukuu - kichwa kinahitaji kuwa chini kidogo kwa sujudu kuliko ilivyo kwa rukuu 'katika nafasi zote za kukaa na kulala

# WAKATI DALILI ZINAPOZIDI KUWA MBAYA

## Fikra Chanya ya Mwenyezi Mungu

Ni muhimu sana kufikiria vyema juu ya Mwenyezi Mungu katika hatua hii ngumu.

Mtume ﷺ amesema:

لَا يَمُوتَنَّ أَحَدُكُمْ إِلَّا وَهُوَ يُحْسِنُ بِاللَّهِ الظَّنَّ

“Wakati wowote mmoja wenu anapokufa, anapaswa kuwa na mawazo mazuri tu ya Mwenyezi Mungu .”

[Saheeh Muslim (2877)]

Wanazuoni wamesema: "kinachomaanisha kufikiria vyema juu ya Mwenyezi Mungu, ni kufikiria kuwa atakuonea huruma na kukusamehe ."

[Sharh Muslim (17/210)]

## Vidokezo vya kukuwezesha kumfikiria vyema Mwenyezi Mungu:

**1.Faida ya kutaka kukutana na Mwenyezi Mungu**

*Mtume ﷺ amesema:* “Mtu anayependa kukutana na Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anapenda kukutana naye.”

[Saheeh Al-Bukhari (6507) & Saheeh Muslim (2684)]

**2. Uchungu utasahaulika kabisa**

*Mtume ﷺ amesema "Siku ya Kiyama, mtu ambaye aliteseka zaidi kutoka kwa wanadamu wote tangu mwanzo hadi mwisho wa nyakati katika suala la uchovu, maumivu, magonjwa, ukandamizaji, kudhoofishwa, udhalilishaji na umasikini. Mtu huyu ataletwa na kuingizwa mara moja katika jannah, na ataambiwa 'Ewe Mwana wa Adamu, je! Umewahi kuona kitu chochote kibaya? Je! Umewahi kupata shida yoyote?' Atasema 'Hapana, ewe Mwenyezi Mungu, Ee Mola. Sijawahi kuona kitu chochote kibaya na sikuwahi kuona shida yoyote”*

[Saheeh Muslim (2807)]

# WAKATI DALILI ZINAPOZIDI KUWA MBAYA

## Vidokezo vya kukuwezesha kumfikiria vyema Mwenyezi Mungu:

**3. Kwa mtu ambaye ametubu kikamilifu, kuondoka kwake kutakuwa kuzuri na kamili na kwa uhakikishio**

*Pia watakutana na wanafamilia ambao walikuwa* waadilifu. Hii inathibitishwa katika mapokeo ya mtume kwamba roho za waumini zinakutana baada ya kifo.

[An-Nasaa'i (1833) & authenticated by Ibn Taymiyyah in Al-Fatawaa (5/449)]

**4. Katika kaburi**

*Mtume ﷺ amesema: "Muumini ambaye atakuwa mtu wa Jannah (ambaye ni pamoja na yule ambaye ametubu kabisa kabla ya yeye kufariki) ataona nafasi yake katika Jannah kila asubuhi na kila jioni wakati akiwa katika kaburi lake."*

[Saheeh Al-Bukhari (1379) & Saheeh Muslim (2866)]

**5. Uwajibikaji kwa siku ya kiyama**

*"Wakati Mtume ﷺ aliona mwanamke aliyepoteza mtoto wake, na alipompata mtoto wake, alimkumbatia na kumnyonyesha. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaambia masahaba: Je, unadhani kwamba mwanamke huyu angemtupa mtoto wake kwenye moto? Tukasema: la Hasha' Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema, 'Mwenyezi Mungu ni mkarimu na mwenye huruma kwa waja wake kuliko vile mwanamke huyu alivyokuwa kwa mtoto wake.""*

[Saheeh Al-Bukhari (5653) & Saheeh Muslim (6921)]

# WAKATI DALILI ZINAPOZIDI KUWA MBAYA

## Vidokezo vya kukuwezesha kufikiria vyema Allah:

**6. Rehema za Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama**

*Mtume* ﷺ amesema: "Mwenyezi Mungu anayo sehemu mia za rehema, ambapo aliteremsha sehemu moja kati ya majini, wanadamu, wanyama na wadudu, ambao kwa njia hiyo wana huruma na rehema kwa mwenzao, kwa njia ambayo wanyama wa porini wana wema kwa watoto wao. Mwenyezi Mungu amebakiza sehemu tisini na tisa za rehema ambazo ataturehemu waja wake Siku ya Kiyama."

[Saheeh Muslim (6908)]

***7. Katika Pepo...***

*Mtume ﷺ atujulisha: "Mnadi* atawaambia watu wa Peponi 'mtakuwa wazima wa afya na hamtawahi kuwa wgonjwa; mtaishi na hamtakufa kamwe; mtakaa vijana na hamtazeeka; mtahisi furaha na hamtasikia kamwe huzuni.'"

[Saheeh Muslim (2827)]

**8. Kama wametubu lakini bado kuhisi kuwa na wasiwasi...**

"*Mtume ﷺAliingia kumuona kijana mmoja alipokuwa akifa, akamwambia, Je!unajisikia vipi? Alisema nina tumaini kwa Mwenyezi Mungu lakini ninaogopa kwa sababu ya dhambi zangu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: "Hizi hisia mbili (woga na tumaini) hazingii moyoni mwa mtu katika hali hii ila Mwenyezi*
*Mungu atampa kile anacho tumaini na amuweke salama kutokana na kile anachohofia."*

[At-Tirmidhi (983) &imethibitishwa na Al-Mundhiree kwenye Targheeb wat Tarheeb (4/214)]]

# HOSPITALINI

## Mambo ya kufanya hospitalini

- Kuwa na subira
- Fikira chanya Mwenyezi Mungu
- Endelea kutafuta msamaha
- Simamisha swala tano kila siku
- Fany du'a na dhikr

## Ikiwa utapona kutoka kwa ugonjwa...

| | | |
|---|---|---|
| **Mshukuru Mwenyezi Mungu** | **Kufanya kusujudu ya kushukrani (Sujood Ash-Shukr)** | **Usiridhike endelea kufanya du'a** |

Ikiwa hali yako haiendi vizuri, endelea kuvumilia, jitahidi kufuata ushauri uliotajwa hapo juu kwenye ukurasa huu, na ujitayarishe kwa uwezekano wa hali kuwa mbaya zaidi.

## Wakati wa hali ikiwa mbaya zaidi

### Kuwa peke yako

Ni muhimu kutambua kwamba, Mwislamu kamwe hayuko peke yake. Kuna malaika wawili (mmoja kutoka nyuma na mmoja mbele) walioteuliwa kulinda muumini hadi wakati wa mtu huyo anaondoka dunia hii.

[Tafseer Ibn Katheer (8/115)]

Mtume ﷺ alituarifu: Wakati wa kufa, kundi kubwa la malaika huleta manukato na sanda nyeupe nzuri kutoka peponi. Malaika wa Kifo ameketi karibu na kichwa cha mwamini, na akasema, 'Ewe roho njema, njoo kwa msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi zake.' Kisha roho hutoka kwa njia ya utulivu sana; malaika huchukua roho kutoka kwa Malaika wa Kifo kisha huiweka katika sanda ya mbinguni na kuipaka manukato ya mbinguni. Baada ya hapo, wanapanda na roho kuelekea mbinguni. Katika anga, roho huungana tena na familia zao waadilifu ambao wamepita mbele yao.

[Sahih Ibn Hibaan & imethibitishwa na Ibn Taymiyah kwenye Al Fatawaa (5/449) & Shu'ab Al-Imaan (1/300) na Al-Baihaqi &imethibitishwa na mwenyewe]

# HOSPITALINI

## Umuhimu wa "Laa ilaha illa-Allah"

*Mtume ﷺ amesema:*

( لَقِّنُوا مَوْتَاكُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ )

*"Waambie wanaokufa waseme Laa ilaaha illa-Allah(hakuna Mungu ila Mungu wa pekee Mwenyezi Mungu)."*

[Saheeh Muslim (916)]

***Umuhimu wa kusema Laa ilaaha illa-Allah kabla ya* umauti**

*Ikiwa kauli ya mwisho ya muumini ni ilaaha* Illa-Allah kabla ya kufa na alikusudia kutubu dhambi zake zote wakati akifanya kauli hii, basi ni matumaini ya dhambi zake zote zitasamehewa. Huu utakuwa mwisho mwema wa maisha yake, ataokolewa kutokana na adhabu na ataingizwa Jannah.

Walakini, hii ni kwa sharti kwamba amerudisha madeni yote aliyopewa na wengine, kifedha au vinginevyo.

[Sharh Muslim by An-Nawawi (1/220)] & [Fathul Bari (3/110) & (10/283)]

**Je, unapaswa kuendelea kurudia "Laa ilaaha illa-Allah"?**

**An-Nawawi amesema:**

*Wanazuoni wanasema*

[Sharh Muslim by An-Nawawi (6/219)]

*Wakati ' Abd-Allah Ibn al-Mubarak alikuwa anakufa, mtu alianza kumkumbusha: "sema, 'Laa ilaaha illa-Allah.'" Mtu huyo aliendelea hadi akazidiwa. Ibn Al-Mubarak akamwambia: " Hakika unachofanya sio kizuri, ninaogopa (ikiwa sikukushauri) kwamba unaweza kumsumbua mwislamu mwingine baada yangu. Wakati wewe unanikumbusha na mimi kujibu na ' Laa ilaaha illa -Allah' na mimi sijasema kitu kingine baadala ya hicho, basi usinikumbushe zaidi. Walakini ikiwa nitasema baada yake maneno mengine, basi nikumbushe tena, ili ' Laa ilaaha illa-Allah ' yaweze kuwa maneno yangu ya mwisho."*

[Siyar A'laam An-Nubalaa (8/418)]

# KUSHUGHULIKA NA KIFO

## Hatua za kwanza za kuchukua wakati unasikia taarifa

### 1. Kuwa mwenye Subira

**Mtume ﷺ amesema:**

إِنَّمَا الصَّبْرُ عِنْدَ الصَّدْمَةِ الْأُولَى

**"(ukweli) subira ni pale tu msiba unapotokea."**

[Saheeh Al-Bukhari (1283) and Saheeh Muslim (926)]

Ibn Hajar amesema kauli hii inamaana:
"Ikiwa mtu anaweza kuonyesha uvumilivu mwanzoni mwa shida wakati wanakaribia kuhisi kuzidiwa na hofu na kutokuwa na uvumilivu, basi huo ni uvumilivu kamili ambao husababisha thawabu."

[Fathul Bari (3/149)]

Wakati wa kusikia juu ya kifo cha mpendwa, mtu anapaswa kujiepusha na chuki kwa Mwenyezi Mungu. Mtu hapaswi:

- Kutoridhika au kuwa na hasira kwa Mwenyezi Mungu au amri zake
- Kuonyesha kutoridhika kwa vitendo vya kupiga mayoe, kushika mashavu yao, kuvua nguo zao au kuvuta nywele zao

Badala yake, mtu lazima awe na uvumilivu:

- Mtu anaweza kupatwa na shida mzito, mateso na chuki lakini wavumilie kwa uvumilivu thabiti
- Wanaweza kutopenda kile wanapitia wakati wa shida, lakini imani yao inawalinda kutokana na kutoridhika

# KUSHUGHULIKA NA KIFO

## Hatua za kwanza za kuchukua wakati unasikia taarifa

### 2. Soma dua ifuatayo

**Dua ya mtume unapopatwa msiba**

إِنَّا لِلّٰهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُوْنَ، اللَّهُمَّ أْجُرْنِي فِي مُصِيْبَتِي وَأَخْلِفْ لِيْ خَيْرًا مِنْهَا

*Innaa lillaahi wa innaa ilayhi raaji'oon.*
*Allaahumma'jurni fee musibatee wa akhlif lee khairan minhaa*

Hakika sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea. Ewe Mwenyezi mungu niruzuku thawabu njema na ubadilishe msiba wangu kuwa yaliyo mema .

Umm Salamah alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema:
Hakuna msiba ambao humsibu mwislamu yeyote na hujibu kwa kusema [du'a ya hapo juu] isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu atamlipa malipo bora kuliko hayo

[Saheeh Muslim (918)]

**Dua ya mtume ya marehemu**

***Kwa Mwanamume:***

اللّٰهُمَّ اغْفِرْ لِ[taja jina la kiume]

وَارْفَعْ دَرَجَتَهُ فِي الْمَهْدِيِّيْنَ، وَاخْلُفْهُ فِيْ عَقِبِهِ فِيْ الْغَابِرِيْنَ، وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهُ يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ، وَافْسَحْ لَهُ فِي قَبْرِهِ، وَنَوِّرْ لَهُ فِيهِ

*Allaahummagh-fir li-(mention name)- warfa' darajatahu fil-mahdiyyeen, wakhlufhu fee 'aqibihi fil-ghaabireen, waghfir lanaa wa lahu yaa rabbal 'aalameen wafsah lahu fee qabrih, wa nawwir lahu feeh.*

***Kwa mwanamke sema:***

اللّٰهُمَّ اغْفِرْ لِ[taja jina la kike]

وَارْفَعْ دَرَجَتَهَا فِي الْمَهْدِيِّينَ، وَاخْلُفْهَا فِي عَقِبِهَا فِي الْغَابِرِينَ، وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهَا يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ، وَافْسَحْ لَهَا فِي قَبْرِهَا، وَنَوِّرْ لَهَا فِيهِ

*Allaahummagh-fir li-(mention name)- warfa' darajatahaa fil-mahdiyyeen, wakhlufhaa fee 'aqibihaa fil-ghaabireen, waghfir lanaa wa lahaa yaa rabbal 'aalameen wafsah lahaa fee qabrihaa, wa nawwir lahaa feeh.*

"Ewe Mwenyezi Mungu! Basi wasamehe fulani au fulani. Na wainue wawe katika watu walio ongoka, na uzitunze na kuzihudumia huduma nzuri familia zao ambazo ameacha nyuma. Ewe Mola mlezi wa walimwengu wote! Basi wasamehe, na utusamehe sisi na umpanulia kaburi yake ) na uweke nuru ndani yake."

[Saheeh Muslim (920)]

# KUSHUGHULIKA NA KIFO

## Hatua za kwanza za kuchukua wakati unasikia taarifa

### 3. Ni kuwaombea maghfira

**Kuwaombea msamaha wazazi na wengine pia**

Mtume ﷺ mesema: “Mtu atainuliwa katika pepo na atauliza 'Hii imetokana na nini?' Na itasemwa kwao 'Kutoka kwa mtoto wako akikuombea msamaha kwa ajili yako.”

[Ibn Maajah (3660) & imethibitishwa na Ibn Katheer kwenye Tafseer yake (7/409)]]

**Ikiwa unajiona na hatia kwamba ulikuwa na mapungufu kwao**

Ibn Taymiyyah amesema:
""Ikiwa mja amepungukiwa kwa kuheshimu wanafamilia, watoto, majirani au ndugu zake, basi anapaswa kuwafanyia du'a kutafuta msamaha."

[Majmoo Al-Fataawa (11/698)]]

### 4. Kutoa sadaka kwa niaba yao

Kuna makubaliano kati ya wanazuoni kwamba sadaka itamnufaisha mtu aliyekufa.

[Sharh Muslim na An-Nawawi (4/70)]

Ni bora kutoa sadaka ya kuendelea kwakuwa itakuwa chanzo cha huruma kwao. Mfano wa miradi endelevu ni miskiti, visima, pampu za maji, nk. Unaweza kuweka ukurasa wa mchango mtandaoni kukusanya michango kutoka kwa marafiki na wanafamilia wengine. Mashirika mengi yanaweza kukusaidia kuweka matangazo kwa niaba yako.


# KUSHUGHULIKA NA KIFO

## Kuwasaidia watu wengine kukabilina na misiba




### 1. Kutoa rambirambi na kuwapa moyo

- Kuhakikisha kwamba miongozo ya kukaa umbali bado unifuatwa




### 2. Kufanya du'a kwa ajili ya marehemu



### 3. Kuwa nao kwenye kipindi hiki kigumu


- Unaweza kuwaunga mkono kuhusu fedha, harakati za mazishi, safari zozote ambazo wanaweza kuhitaji msaada nazo
- Kutoa msaada wa kihisia na kuwafariji
- Msiwape mizigo/usumbufu





### 4. Toa sadaka kwa niaba yao

[Sharh Muslim by An-Nawawi (4/70)]



### 5. Fanya utaratibu kuwapatia chakula

- Fanya hivi kwa wakati unaofaa kwao na kwa idhini yao
- Kupeana chakula nyumbani kwa yule aliyefariki ilikuwa ni mazoea ya yaliyoyiliwa nguvu na Mtume ﷺ

[At Tirmidhi (998) At Tirmidhi (998) & imethibitishwa na mwenyewe]

# TARATIBU ZA MAZISHI

**Ibn Qudamah amesema:**

"Kuhusu mtu aliye na thawabu za shahidi ambaye hakuuawa, kama vile mtu aliyekufa na ugonjwa wa tumbo, yule aliyekufa kwa kupooza, yule aliyezama, mmoja aliyeangamizwa na ukuta ulioanguka na yule mwanamke aliyekufa wakati wa kujifungua, zinapaswa kuoshwa na swala ya jeneza iswaliwe ajili yao. Hatujui tofauti yoyote ya maoni ya wanazuoni juu ya hatua hii..."

[Al-Mughni (2/204)]

## Kuosha mwili wa marehemu*

- Mahitaji ya chini ya kuosha mwili ni maji kufikia kila sehemu ya mwili wa marehemu.

  [Al-Mabsoot (2/229), Al-Fawakih Ad-Dasani (2/668), Tuhfatul Muhtaj (3/98) & Kashaf Al-Qinaa (2/93)]
- Kama kuna hofu kwamba watu wataambukizwa ugonjwa wakati kuosha mwili, basi wanapaswa kufanya hivyo kwa tahadhari wakati wamevaa vifaa sahihi vya kinga.
- Kama mwili hauwezi kuoshwa, tayammum na udongo/jiwe lazima kufanyika .

## Kukafini*

- Sharti la chini la kufunika mwili ni kipande kimoja cha kitambaa ambacho hufunika mwili mzima .


  [Saheeh Al-Bukhari (4047), Saheeh Muslim (940), Haashiya Ibn 'Aabideen (3/98); Mawaahib Al-Jaleel (2/266); & Al-Mughni (3/386)]
- Ikiwa hakuna kitambaa cha kutosha basi funika mwili sehemu kubwa iwezekanavyo, hakikisha kwamba maeneo ya siri yanahifadhiwa.

*Tafadhali kumbuka: shughuli za kuosha na kuvisha sanda (zinaweza kutofautiana kulingana na sehemu na eneo husika. Tafadhali fuata miongozo ya usalama wakati wa kuhakikisha kuwa haki za kidini zinatekelezwa kwa usahihi.

# TARATIBU ZA MAZISHI

## Jinsi ya kuswali swala ya jeneza

### Jinsi ya kuswali swala ya jeneza



1. Simama na sema "Allahu akbar"
2. Kisha soma Surah Al-Fatihah au du'a ya ufunguzi wa swala inayoitwa Thanaa au Istiftah
3. Kisha sema 'Allahu akbar' mara ya pili
4. Ikifuatiwa na Allaahumma salli 'alaa (Ibrahimiyyah/durood sharif)
5. Kisha sema 'Allahu akbar' kwa mara ya tatu
6. Kisha soma dua ifuatayo ya Mtume:

**Kwa wanaume:**

اللّٰهُمَّ اغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ، وَعَافِهِ وَاعْفُ عَنْهُ ، وَأَكْرِمْ نُزُلَهُ ، وَوَسِّعْ مُدْخَلَهُ ، وَاغْسِلْهُ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ، وَنَقِّهِ مِنَ الْخطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الْأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ ، وَأَبْدِلْهُ دَارًا خَيْرًا مِنْ دَارِهِ ، وَأَهْلًا خَيْرًا مِنْ أَهْلِهِ، وَزَوْجًا خَيْرًا مِنْ زَوْجِهِ، وَأَدْخِلْهُ الْجَنَّةَ ، وَأَعِذْهُ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَ عَذَابِ النَّارِ

Allaahummaghfir lahu warhamh, wa 'aafihi wa'fu 'anh, wa akrim nuzulah, wa wassi' mudkhalah, waghsilhu bilmaa'i waththalji walbarad, wa naqqihi minalkhataayaa kamaa naqqaytath-thawbal-'abyada minad-danas, wa 'abdilhu daaran khayran min daarih, wa 'ahlan khayran min 'ahlih, wa zawjan khayran min zawjih, wa 'adkhilhul-jannah, wa 'a'idhhu min 'adhaabil-qabri wa 'adhaabin-naar.

[Saheeh Muslim (963)]

**Kwa wanawake:**

اَللّٰهُمَّ اغْفِرْ لَهَا وَارْحَمْهَا ، وَعَافِهَا وَاعْفُ عَنْهَا،وَأَكْرِمْ نُزُلَهَا، وَوَسِّعْ مُدْخَلَهَا، وَاغْسِلْهَا بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ، وَنَقِّهَا مِنَ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الْأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ ، وَأَبْدِلْهَا دَارًا خَيْرًا مِنْ دَارِهَا ، وَأَهْلًا خَيْرًا مِنْ أَهْلِهَا، وَزَوْجًا خَيْرًا مِنْ زَوْجِهَا، وَأَدْخِلْهَا الْجَنَّةَ ، وَأَعِذْهَا مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَعَذَابِ النَّارِ

Allaahummaghfir lahaa warhamhaa, wa 'aafihaa, wa'fu 'anhaa, wa akrim nuzulahaa, wa wassi' mudkhalahaa, waghsilhaa bilmaa'i waththalji walbarad, wa naqqihaa minalkhataayaa kamaa naqqaytath-thawbal-'abyada minad-danas, wa 'abdilhaa daaran khayran min daarihaa, wa 'ahlan khayran min 'ahlihaa, wa zawjan khayran min zawjihaa, wa 'adkhilhal-jannah, wa-a'idhhaa min 'adhaabil-qabri wa 'adhaabin-naar

[Saheeh Muslim (963)]

# TARATIBU ZA MAZISHI

## Swala ya jeneza

**Tafsir ya dua ya mazishi:**

"Ewe Mwenyezi Mungu msamehe na umrehemu na umpe kinga . Ewe Mwenyezi Mungu kuwa mkarimu kwake na mapanulie makazi yake, na msafishe na maji, theluji na barafu. Ewe Mwenyezi Mungu msafishe makosa yake kama madoa yanvyotoka kwenye nguo nyeupe.
Mpe makaazi bora kuliko nyumba yake, na familia bora kuliko familia yake na mwenza bora kuliko mwenza wake. Mchukue Peponi na umlinde kutokana na adhabu ya kaburi na kutoka kwa adhabu ya Motoni."

[Saheeh Muslim (963)]

7. Kisha sema "Allahu akbar " kwa mara ya nne

[Musnad Ash-Shaafi'ee (588) & authenticated by Al-Baihaqi in As-Sunan Al-Kubra (4/39)]

8. Kisha sema "Assalamu'alaykum wa rahmatullah" mara moja kulia kwako unaweza pia kufanya kushoto kumaliza kumaliza swala

### Hoja zaidi juu ya swala ya jeneza

- Inawezekana kwamba swala ya jeneza ikafanyikia kaburini.
- Idadi ya chini ya watu wanaohitajika kwa swala ya jeneza ni Muislamu mmoja. [Fathul Mun'im (4/243)]
- Barakoa zinaweza kuvaliwa wakati wa kufanya swala.
- Kuacha nafasi kati ya waumini pia ni halali wakati wa majanga.
- Kauli ya Mtume imesema: Wakati wowote muislam akifa na waislam 40 ambao hawamshirikishi Mwenyezi Mungu wakafanya swala ya jeneza juu yake, Mwenyezi Mungu atawaruhusu kumuombea msamaha kwa niaba yake, (Maana yake atakubali dua yao na kumsaheme marehemu). [Saheeh Muslim (948)]
- Hata hivyo, kama haiwezekani kwa watu 40 kuhudhuria kwa sababu ya kanuni zilizopo, basi ni matumaini kwamba bado watapata nguvu hiyo kwa idadi ya watu watakaoruhusiwa kuhudhuria.
- Kama haiwezekani kuwa na mwili wakati wa swala ya jeneza, kutokana na karantini au vikwazo vingine, na hakuna mtu amefanya maombi ya mazishi juu ya mwili, basi wanazuoni kadhaa wameruhusu swala ya jeneza kuswaliwa bila kuwepo kwa mwili.

[Saheeh Al-Bukhari (3877) & Saheeh Muslim (952)]

# TARATIBU ZA MAZISHI

## Kuzika

- Hakuna idadi ya chini ya watu wanaohitaji kuzika waliofariki, kutoka kwa mtazamo wa Kiislamu. Kadri mazishi yakifanyika basi jukumu limetimia

  [Al-Ijmaa by Ibn Al-Mundhir (p. 52)]

- Kuzikwa miili mingi katika kaburi moja inaruhusiwa, kama inahitajika kufanya hivyo. Kuna mifano ya wakati wa Mtume ﷺ alifanya hivyo . Kwa hivyo basi, ikiwa utaona hii ikitokea kwenye kaburi ujue ni halali.

  [Al-Majmoo' by An-Nawawi (5/247) & Saheeh Al-Bukhari (1343)]

- Haipendekezwi kuzika mwili katika jeneza kulingana na makubaliano ya wazuoni. Walakini, inaruhusiwa ikiwa ni kwa sababu ya lazima.

  [Mughni Al-Muhtaj (1/539)]

- Mwili unapaswa kuwekwa kwenye kaburi upande wake wa kulia, ukitazamana na qiblah. [Al-Muhala by Ibn Hazm (5/173)]

## Baada ya mazishi

- Mtume ﷺ amesema: "Mwombeeni msamaha ndugu yenu, na muombe Mwenyezi Mungu ndugu yenu abaki thabiti (katika kujibu maswali y malaika wawili) kwa sasa anahojiwa."

  [Abu Dawood (3221) & imethibitishwa na An-Nawawi kwenye Al-Majmoo (5/291)]

At-Tirmidhi amesema:

- "Maombi ya mazishi na kufanya du'a kwa marehemu baada ya mazishi ni aina ya msaada kwao, kwani kundi la Waislamu wanaoswali swala ya jeneza ni kama kupeleka askari ambao wamekusanyika nje ya mlango wa Mfalme, wakimwombea. Halafu, tukisimama karibu na kaburi lake, kumuombea abaki thabiti ni kama kuwasaidia askari zaidi kwani huu ni wakati ambao marehemu yuko mikononi mwa wamiliki, kwani kwa sasa anakabiliwa na hali ya kutisha kwa kuhojiwa na malaika.

  [Haashiyat Ar-Rawd by Ibn Al-Qassim (3/124])

# BAADA YA MAZISHI

## Kuzuru makaburi

### Du'a  Mtume ya kuzuru makaburi

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ ، وَإِنَّا إِنْ شَاءَ اللَّهُ بِكُمْ لَلَاحِقُونَ،
وَيَرْحَمُ اللّٰهُ الْمُسْتَقْدِمِيْنَ مِنَّا وَالْمُسْتَأْخِرِيْنَ، أَسْأَلُ اللّٰهَ لَنَا وَلَكُمُ الْعَافِيَةَ

Assalaamu'alaykum 'ahlad-diyaari minal-mu'mineena walmuslimeen, wa 'innaa 'in shaa' Allaahu bikum lalaahiqoon, wa yarhamullaahul-mustaqdimeena minnaa walmusta'khireen, as'alul-laaha lanaa wa lakumul-'aafiyah

*Assalamu'alaykum, Enyi* wenyeji wa makaburini, waumini na Waislamu. Hakika tutaungana nanyi hivi karibuni insha Allah. Mwenyezi Mungu atuhurumie sisi tunaoendelea na wale watakaokuja. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe uzima na usalama

[Sahih Muslim (974) & (975)]

"*Assalamu'alaykum*" hapa inamaanisha ulinzi kutoka kwa adhabu wanazopata wenyeji wa makaburini, kwa vile mtu anaweza kuadhibiwa kaburini hata ikiwa ni kiasi kidogo. Kwa hivyo, unapomuomba Mwenyezi Mungu kinga kwa ajili yake, atalindwa

[Sharh Al-Mumti' (5/259)]

# NENO LA MWISHO

*Jazakumullahu* khairan kwa kufikia mwisho. Tunaomba Mwenyezi mungu yaliyomo kwenye kijitabu hiki yawe ni ya faida kwako wewe na wapendwa wako. Ikiwa unayo maoni, marekebisho au maswali yoyote kuhusu yaliyomo kwenye kijitabu hiki basi tafadhali tutumie barua pepe kwa info@spiritualantidote.com. Tutafurahi kusikia kutoka kwako. Tunaweza pia kuchapisha  kijitabu hiki kufuatia maombi yako.

Tunaomba Mwenyezi Mungu awalinde ninyi na familia zenu wakati huu. Mwenyezi Mungu awahurumie wote waliotangulia mbele ya haki na awaingize Jannah. Tunaomba atusamehe mapungufu yetu yote, na afanye jaribio hili kuwa njia kwetu kupata ukaribu wake na maridhio yake. Ameen.